RISING STAR EXAMINATION SERIES

# DARASA LA SITA

## MWAKA WA 2021

## KISWAHILI SEHEMU YA KWANZA: LUGHA

Dedicated to Excellence

**JINSI YA KUTUMIA KARATASI YA MAJIBU**

**Muda: Saa 1 dakika 40**

1. Tumia penseli ya kawaida tu.
2. Hakikisha umeandika kwa karatasi ya majibu:-
   ***(i) JINA LAKO*** ***(ii) JINA LA SHULE YAKO***
3. Kwa kila swali onyesha kwa kupiga mstari kwenye mabano lile jibu ulilolichagua limeandikwa.

***Kifungu kifuatacho kina nafasi 1-15. Jaza kila nafasi kwa jibu lifaalo zaidi kati ya uliyopewa hapo chini.***

Upweke ni __1__. Mwanadamu __2__ kuishi peke yake __3__ ni watu. Kwa hivyo ni vyema __4__ haja ya ushirikiano __5__ ya watu wa tabaka mbalimbali __6__ wa aina __7__ haufai __8__.

| | | | | |
|---|---|---|---|---|
| **1.** | A. hasara | B. dhambi | C. uvundo | D. mapenzi |
| **2.** | A. hakuumbwa | B. hakuundwa | C. hakutengwa | D. hakuungwa |
| **3.** | A. Mungu | B. yeye | C. malaika | D. mtu |
| **4.** | A. kuthamini | B. kudhamini | C. kudhamiria | D. kutathmini |
| **5.** | A. kando | B. fauka | C. baina | D. licha |
| **6.** | A. uuguzi | B. ubaguzi | C. uvamizi | D. unyamavu |
| **7.** | A. lolote | B. yoyote | C. wowote | D. chochote |
| **8.** | A. kuendelezwa | B. kuondolewa | C. kuendewa | D. kuondoshwa |

Kwa bahati __9__ kumbe hatukuwa __10__ na barabara. Mara tuliona __11__ wa gari. Tulipumua kwa gari __12__ kusimama na babu akatuita __13__ gari. Tulifika nyumbani salama __14__ kweli __15__.

| | | | | |
|---|---|---|---|---|
| **9.** | A. nzuri | B. mzuri | C. zuri | D. vizuri |
| **10.** | A. kando | B. mkabala | C. mbali | D. nje |
| **11.** | A. mmuliko | B. mmiminiko | C. mngummo | D. mchakato |
| **12.** | A. hiyo | B. hilo | C. huo | D. hizo |
| **13.** | A. tulishuka | B. tuling'oa | C. tulitoka | D. tuliabiri |
| **14.** | A. salilima | B. salamu | C. salmini | D. salimu |
| **15.** | A. tuliponea chupuchupu | B. tuliona cha mtema kuni | C. tuliona aibu | D. tuliona wivu |



Compiled& distributed by Schools Net Kenya, P.O. Box 15509-00503, Nairobi | Tel:+254202319748 E-mail: infosnkenya@gmail.com | ORDER ANSWERS ONLINE at www.schoolsnetkenya.com

***Kutoka swali la 16-30, chagua jibu kulingana na maagizo***

16. Tumia kiashiria radidi kifaacho kukamilisha sentensi hii.

Yai _____ ndilo nililolinunua.

A. hii hii | B. hili hili
C. lili hili | D. ii hii

17. Kinda ni kwa ndege kama vile _______ ni kwa kipepeo.


A. buu | B. kisuse
C. kiluwiluwi | D. kiwavi

18. ***Tumia amba kukamilisha sentensi ifuatayo.***

Tundu _____ huwa ukutani husababisha nyufa.

A. ambalo | B. ambazo
C. ambayo | D. ambacho

19. Umbo hili linaitwaje?



A. Mchemraba
B. Mchemstatili
C. Hori
D. Mraba

20. ***Kamilisha methali:***

Siri ya mtungi aijuaye ________

A. maji | B. mwenye kiu
C. mtekaji | D. kata

21. ***Kamilisha sentensi ifuatayo kwa kutumia enye.***

Uovu ________ ulitendewa wananachi.

A. yenyewe
B. wenyewe
C. zenyewe
D. mwenyewe

22. Chagua tashbihi inayofaa kukamilisha sentensi.

Wale pacha wanafanana kama ______

A. kope na macho | B. shilingi kwa ya pili
C. kinu na mchi | D. sahani na kawa

23. ***Andika wingi wa.***

Chuma cha gari kimevunjika.

A. Chuma za magari zimevunjika
B. Vyuma vya magari vimevunjika
C. Machuma ya magari yamevunjika
D. Vyuma za gari zimevunjika

24. Ni sentensi gani iliyo katika wakati timilifu?

A. Ndovu waliharibu mashamba ya wakazi
B. Samaki wengi watavuliwa kesho
C. Mbunge wetu amechaguliwa tena
D. Wageni wetu wanaondoka asubuhi

25. $^4/_9$ kwa maneno ni:-

A. ushuri nne
B. subui nne
C. tusui nne
D. thumni nne

26. ***Kanusha sentensi ifuatayo:***

Walifika na wakaonana

A. walifika lakini hawakuona
B. Walionana walipofika
C. Hawakufika wala hawakuonana
D. Hawakufika ingawa walionana

27. Siku iliyotangulia jana ni ________

A. kesho | B. mtondo
C. kitojo | D. juzi

28. Nomino uzi, ukuta, wimbo, wakati ni ngeli gani?

A. U-ZI | B. U-I
C. U-U | D. I-ZI

29. Andika katika hali ya kutendewa. Lea

A. lelewa | B. lewa
C. lewesha | D. lelea

30. ***Tegua kitendawili kifuatacho***

Kipo lakini sikioni ________

A. redio | B. kioo | C. upepo | D. kisogo



Compiled& distributed by Schools Net Kenya, P.O. Box 15509-00503, Nairobi | Tel:+254202319748 E-mail: infosnkenya@gmail.com | ORDER ANSWERS ONLINE at www.schoolsnetkenya.com

***Soma shairi lifuatalo kisha ujibu maswali 31-40.***

Mwalimu ninalo swali, naomba yako lisani,
Unipe jibu sahali, name na yakini,
Menisumbua akili, jibu sijalibaini,
Kiini chake ni nini, rangi za bendera yetu?

Kijana sibabaike, jaribu kutulizana,
Uketi umakinike, tupate kwelezana,
Nikwambie upulike, sababuye na maana,
Bendera yetu kijana, rangize ni kumbukumbu.

Nitafurahi mwalimu, ukiniambia kiini
Kwani bado sifahamu, ni za kumbukumbu gani?
Zilizokuwa muhimu, za kukumbukwa nchini,
Kiini chake ni nini, rangi za bendera yetu?

Rangi nyeusi hakika, kwetu ni maana sana,
Rangi ya mwafrika, mno nayo twajivunia,
Rangi isofananika, pekee yaonekana,
Bendera yetu kijana, rangize ni kumbukumbu.

Nyeupe uionayo, inayo yake maana,
Yaonyesha zetu nyoyo, ni nyeupe twapendana,
Tu mbali mno na choyo, kinyongo pia hatuna,
Bendera yetu kijana, rangize ni kumbukumbu.

Kijana rangi nyekundu, rangi ya huzuni sana,
Watu mepiga nyekundu, na mishale kufumana,
Kwa damu matundu tandu, uhuru mepatikana,
Bendera yetu kijana, rangize ni kumbukumbu.

Rangi ile kijani, yaonyesha tutanona,
Kuwa hapana nchini, rutuba imejazana,
Mazao tele shambani, tulimayo na kuvuna,
Bendera yetu kijana, rangize ni kumbukumbu.

Yatosha nimefahamu, lengo na chake kiini,
Ya kuwa yetu alamu, ni chombo chenye thamani,
Nakushukuru mwalimu, kunitoa ujingani,
Bendera yetu kijana, ni chombo cha ukumbusho

**31.** Shairi hili ni la aina gani?
A. Tarbia B. Tathlitha
C. Takhimisa D. Tathnia

**32.** Shairi hili ni la majibizano kati ya:-
A. mwalimu na bendera
B. kijana na rangi
C. mwalimu na kijana
D. mwalimu na rangi

**33.** Shairi hili lina mishororo mingapi?
A. 4 B. 32
C. 60 D. 40

**34.** Ubeti wa saba unaongea kuhusu nini?
A. Mwanafunzi anauliza kuhusu tangi ya kijani
B. Mwalimu anauliza kuhusu rangi ya kijani
C. Mwalimu aeleza kuhusu rangi ya kijani
D. Mwalimu anaeleza kuhusu rangi nyeupe

**35.** Ni rangi gani inayoonyesha nyoyo zetu?
A. Nyeupe B. Kijani
C. Nyeusi D. Nyekundu

**36.** Taja vina vya kati na vya mwisho katika ubeti wa sita.
A. ndu, na
B. na, ndu
C. yo, na
D. mu, ni

**37.** Anayetunga mashairi na kuyaimba huitwa ______
A. manju
B. mghani
C. tarishi
D. malenga

**38.** Ni rangi gani ambayo inaonyesha rangi ya mwafrika?
A. Nyeusi
B. Kijani
C. Nyeupe
D. Nyekundu

**39.** Shairi hili linaongea kuhusu:-
A. kupigania uhuru kwa mwafrika
B. amani tuliyo nayo pamoja na upendo
C. rangi za bendera na maana zake
D. nchi yenye rutuba

**40.** Kibwagizo cha ubeti wa sita ni kipi?
A. Kiini chake ni nini, rangi za bendera yetu
B. Bendera yetu kijana, rangize ni kumbukumbu
C. Rangi isofananika, pekee yaonekana
D. Tu mbali mno na choyo, kinyongo pia hatuna



Compiled& distributed by Schools Net Kenya, P.O. Box 15509-00503, Nairobi | Tel:+254202319748 E-mail: infosnkenya@gmail.com | ORDER ANSWERS ONLINE at www.schoolsnetkenya.com

***Soma taarifa ifuatayo kisha ujibu maswali 41-50.***

Kobe alitamani kubadili maskani yake. Basi akamwomba tai amchukue mpaka kwenye mastakimu yake mapya. Akaahidi kumpa ujira wake. Tai akakubali. Akamkamata kobe gamba lake akapaa naye juu sana. Jioni wakakutana na kunguru. Akamwambia tai, "bwana wee, huna habari huyo kobe anafaa sana kwa chakula, dhihaka mbali." Tai akajibu akamwambia, ndiyo, bwana lakini gamba lake ni gumu mno."

Kunguru akamwambia, "Ahh! Hilo si neno. Mwamba waweza kulipasua mara moja wala siyo kazi kubwa."

Basi tai akafuata shauri la kunguru, akambwaga kobe penya mwamba. Ndipo wale ndege wawili wakafaidi kula chakula chao ndicho kobe.

**41.** Kobe alitamani kufanya nini?

A. Kuchukuliwa na tai
B. Kubadili mastakimu mapya
C. Kuhamia maskani mapya
D. Kuhama maskani mapya

**42.** Tai angelipwa ujira wake

A. kabla hajamchukua kobe
B. punde tu angekubali kumbeba kobe
C. angemfikisha kobe salama katika makao mapya
D. baada ya kumfikisha kobe katika maskani yake

**43.** Tai alikubali kumchukua kobe kwa sababu ______

A. alitaka kumla
B. aliahidiwa malipo
C. alijua ni chakula kinachofaa
D. alitaka kubwaga mwambani

**44.** "Dhihaka: ni sawa na:-

A. mzaha
B. uongo
C. wahaka
D. haraka

**45.** Kunguru na tai:-

A. wote ni ndege walao matunda
B. ni ndege wala mizoga
C. ni ndege wanaozaa watoto
D. wanaishi pamoja

**46.** Neno lenye maana sawa na maskani ni:-

A. kiota
B. chengo
C. pango
D. makavazi

**47.** Gamba kwa kobe ni sawa na ______ kwa mti.

A. gome
B. ganda
C. utando
D. ngozi

**48.** "Ali" ni tambo la kishangao kinachotumiwa:-

A. kuonyesha furaha
B. kuonyesha tukio la kukera
C. kushangilia
D. kuitikia jambo

**49.** Kunguru alimaanisha nini aliposema "hili si neno?"

A. Kobe hana taabu
B. Ugumu wa gamba la kobe hauwezi kuwazuia kumla
C. Kobe hana la kufanya
D. Gamba la kombe si gumu

**50.** Habari hii inatufunza nini?

A. Kobe ni mnyama asiyemwerevu
B. Usimwamini adui wa jadi hata kama una dhiki
C. Kunguru ana akili kuliko tai
D. Tai ni ndege mwenye nguvu



Compiled& distributed by Schools Net Kenya, P.O. Box 15509-00503, Nairobi | Tel:+254202319748 E-mail: infosnkenya@gmail.com | ORDER ANSWERS ONLINE at www.schoolsnetkenya.com